**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**

**SHULE YA SEKONDARI MAHIDA**

**NAMBA ZA SIMU**

0759509194/ 0624031470– Mkuu wa Shule.

0765959820– Makamu Mkuu wa shule. ,

Email: mahisecondary@yahoo.com

SHULE YA SEKONDARI MAHIDA

S.L.P 432,

**MKUU – ROMBO.**

**Tarehe: …………….**

Mzazi/Mlezi/Mfadhili wa Mwanafunzi:……………………………………………………………

S.L.P……………………………………………..

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAHIDA HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO MKOA WA KILIMANJARO MWAKA …………..</u>**

**1.** Nafurahi kukujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga katika Shule ya Sekondari Mahida kidato cha Tano kwa mwaka huu wa ……………… na atasoma tahasusi ya………………….. .Shule ipo umbali wa kilomita 48 kutoka **Moshi mjini Kilimanjaro**. Usafiri wa gari kutoka Moshi mjini hadi Rombo unapatikana katika kituo cha mabasi cha **Moshi Mjini**. Nauli ya kutoka Moshi mjini hadi Mkuu Rombo ni Tshs. 4000 hadi Tshs. 5000 kutegemea na gari. Kwa wanafunzi wanaotoka Dar es Salaam au kupitia Dar es Salaam wapande magari ya Dar express, Tilisho, Esther luxury, King Meridian; yanayokuja moja kwa moja Rombo. Kwa wanaotoka Dodoma wapande Shabiby, Extra coach au Ngasere na wanaotoka Singida wapande Mtei express. Kwa wanaotoka Mwanza na maeneo mengine ya kanda ya ziwa wapande mabasi yanayofika hadi moshi mjini na kisha kupanda usafiri mwingine hadi shuleni. Kwa wanafunzi wote kituo cha kushukia baada ya kutoka Moshi mjini ni **MAMSERA** na baada ya hapo atapanda usafiri wa pikipiki kuelekea shuleni kwa gharama ya Tsh 4,000/=. Muhula wa masomo unaanza tarehe ………….. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shulenitarehe ………….. mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………….** (Kulingana na maelekezo yatayotolewana na mamlaka husika)

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2.1 SARE ZA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa maadili ya mwanafunzi awapo shuleni. **Nguo za kubana na fupi ni marufuku na mwanafunzi hatapokelewa.** Sare ni kama ifuatavyo

**<u>KWA WASICHANA</u>**

i. Sketi mbili (02) rangi ya **<u>SKY BLUE</u>** inayozidi magoti kwa urefu unaokaribia kwenye viatu. mshono – **"Rinder box" mbele na nyuma pembeni marinda madogomawili.**
ii. Mashati mawili (02) ya mikono mirefu.
iii. Sare ya Michezo ni **truck suit nzito rangi ya dark blue na jezi ya rangi maroon (damu ya mzee) na bukta yake (isiwe na maandishi yeyote) pamoja na raba nyeusi za michezo (na njumu kwa watakaocheza mpira wa miguu).**
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; (zingatia sana kuhusu aina ya viatu)
v. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
vi. Sweta **la Shule zito la rangi ya sky blue** yenye kola ya "V.(Inashauriwa mtoto kuwa na sweta mbili). Pia yanaweza kupatikana shuleni kwa gharama ya tsh 12,000/=
vii. Magauni mawili ya kushindia (*shamba dresses*) yenye drafti ya rangi ya dark blue na nyeupe yakiwa na mshono wa solo, yawe marefu kugusa kisigino. Pia yanaweza kupatikana shuleni kwa gharama ya tsh 25,000/= kwa moja.
viii. Tai ndefu rangi ya sky blue
ix. Mabuti (rain boots)rangi nyeusi
x. Tisheti (T-shirt) **nzito rangi ya Dark Blue (form six) inapatikana shuleni.**

Kwa maelekezo zaidi ya kuhusu sare angalia picha hapo chini.









**KWA WAVULANA**

i. Suruali mbili (02) rangi ya **sky blue** ziwe na marinda mawili na chini isipungue nchi 15 (Mzunguko wa chini uwe na Turn up)

ii. Mashati mawili (02) ya mikono mirefu.

iii. Sare ya Michezo **ni truck suit nzito rangi ya dark blue na jezi ya rangi ya maroon (damu ya mzee) na bukta yake ( zote zisiwe na nembo au maandishi yeyote) pamoja na raba nyeusi za michezo (na njumu kwa watakaocheza mpira wa miguu).**

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; (zingatia sana kuhusu aina ya viatu)

v. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vi. Sweta **la Shule zito Rangi ya sky blue** yenye kola ya "V**. (Inashauriwa mtoto kuwa na sweta mbili).**

vii. Nguo za **kushindia (*shamba dress*) ni suruali mbili (2) nyeusi na T-shirt nyekundu zenye kola (maarufu kama form six)**

viii. Tai ya rangi ya sky blue

ix. Mabuti (Rain boots) rangi nyeusi.

x. Tisheti (T-shirt) **nzito rangi ya Dark Blue (form six). Pia zinapatikana shuleni zikiwa na nembo**









**<u>NB:</u> Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo au viatu vyovyote tofauti na vilivyoainishwa kwenye fomu hii na pia mwanafunzi akija na sare tofauti na inayohitajika hatopokelewa, hivyo basi endapo mzazi atapatwa na mashaka kuhusu rangi ya sare za shule awasiliane na Mkuu wa Shule au Makamu Mkuu wa Shule namba zimewekwa kwenye fomu hii.**

### 2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA KUJA NAYO SHULENI KWA WOTE

i. Madaftari kubwa (Counter book) kumi (10)
ii. Ream 2 ya karatasi nyeupe A4.
iii. Ream 2 Ruled Paper (yenye mistari)
iv. Wanafunzi waje na vitabu vifuatavyo kulingana na Tahasusi aliyochaguliwa

| Na | Somo | Vitabu |
|---|---|---|
| 1 | HISTORY | a) Advanced Level History form 5 and 6 by TIE<br>b) History for High Schools form five and six by Bakari Madaya<br>c) Advanced History 1& 2 by Saleh Yassin<br>d) Advanced Level History form 5 and 6 by Msuya |
| 2 | LANGUAGE | a) Mastering Advanced level English by Alex Mkunda<br>b) English for Advanced Secondary Schools Form five by TIE<br>**<u>PLAYS</u>**<br>a) Animal form by George Orwel<br>b) Chasing the leopard finding the lion by Julie Wakimam - Linn<br>c) The Opportunist by Nyambari C. Nyangwine<br>d) The Horizon Unveiled by Followes Mwaisela<br>**<u>NOVELS</u>**<br>a) The government inspector by Nikolai Gogol<br>b) An enermy of the people by Henrik Ibsen<br>c) A taste of heaven by Faronk Topan<br>**<u>POEMS</u>**<br>a) Summons by Richard S. Mabala<br>b) Poets of Africa: Lament of the silent & other poems by East African Educational publisher |
| 3 | GEOGRAPHY | a) Practical geography Alive by Zisti<br>**b)** Physical Geography and Land Appreciation<br>**c)** Physical Geography by Bunnet B.<br>d) Physical Geography 5 and 6 by TIE<br>e) Practical Geography by TIE |
| 4 | CHEMISTRY | i). Physical chemistry (curriculum) TIE<br>ii).General and Inorganic chemistry TIE<br>iii). Organic chemistry TIE |
| 5 | BIOLOGY | a) .Biological Science (BS Green) Green, N. P. O., Stout, G. W., & Taylor, D. J. (2001). Biological science. Cambridge University Press.<br>b) TIE. (2024). Biology for secondary schools student's book form five. Tanzania Institute of Education.<br>c) TIE. (2025). Biology for secondary schools student's book form six.<br>d) Understanding BiologyToole, G., & Toole, S. (1999). Understanding biology for advanced level. Stanley Thornes Publishers. |

v. Dissecting kiti kwa wanafunzi wa Biolojia (Mwanafunzi anayesoma anapaswa kununua) itakaguliwa wakati akifika shuleni.
vi. Scientific calculator (hii ni kwa wanafunzi wote)
vii. Kalamu za kutosha, penseli na rula pamoja na mathematical set.
viii. Shuka mbili rangi ya Pink kwa wasichana na rangi ya sky blue kwa wavulana na Blanketi la shule moja, mto na foronya
ix. Godoro la $2\frac{1}{2}$ " x 6 kwa wavulana na 3" X 6 kwa wasichana
x. Masweta mazito wawili meusi ya kushindia yasiyo na kofia wala nembo au maandishi yoyote.
xi. Tochi isiyo ya kuchaji kwa ajili ya kutumia pindi umeme ukikatika.
xii. Mizula (boshori) nyeusi zisizo na maandishi au nembo yoyote.
xiii. Vyombo vya chakula: Sahani, Bakuli, Kijiko na Kikombe (Vinapatikana eneo la shule kwa wale wasiokuja navyo)
xiv. Vifaa vya usafi binafsi miswaki, sabuni, dawa ya meno, brush la miguu na viatu pamoja na kiwi.
xv. Ndoo mbili ndogo (lita kumi) zenye mifuniko na kandambili za kuogea (Atanunua akiwa shuleni kwa anayehitaji)
xvi. Nguo za ndani za kutosha;
xvii. Wavulana watapaswa kuleta sabuni ya maji lita 5, jembe na pini wake
xviii. Wasichana watapaswa kuleta sabuni ya maji lita 5, kwanja 1 na squizer 1
**xix. Wanafunzi wote wanapaswa kuwa na bima ya afya ambazo pia zinaweza kupatikana shuleni kwa utaratibu maalumu.**

## 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| | Tahadhari | 5,000/= |
| | Nembo | 5,000/= |
| | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:**

Michango mbalimbali iliyotajwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti ya **shule MAHIDA SECDONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT 40401100036 NMB . Hatupokei fedha taslimu malipo yote yafanywe kupitia benki**. Unaweza kulipia michango hiyo popote kwenye tawi la NMB. Baada ya kufanya malipo hayo Mwanafunzi au mzazi anatakiwa kuleta "Bank Pay In Slip shuleni siku ya kuripoti ili aweze kukatiwa stakabadhi ya Serikali kwa malipo aliyoyafanya na kusajiliwa.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatumia simu ya Patron (kwa wavulana) na matron (kwa wasichana), endapo mwanafunzi atatumia simu nyingine itatafsiriwa kuwa kosa la utovu wa nidhamu linaloweza kupelekea mwanafunzi kufukuzwa shule.**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**N.B;***Mzazi/mlezi utalazimika kufika shuleni pindi mwanao abainikapo kuwa na makosa hayo na utaondoka naye kwenda nyumbani.*

### 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

...............................

**ELIFARIJI H. MIRARO**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MAHIDA
S. L. P. 432
MKUU – ROMBO

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0759509194/ 0624031470**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0765959820**
- **Mwandamizi Taaluma 0719575602**
- **Mwandamizi Malezi 0787934435**

**Kiambatanisho A.**

## SHULE YA SEKONDARI MAHIDA

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

A: Jina ……………………………………………………………………………………………………

Tarehe ya kuandikishwa ……………………………….. na. ……..........................………………………

Tarehe ya kuzaliwa ……………………………….. Mwaka ………………………………..

Taifa …………………………………….. Mkoa …………….………… Wilaya ………………………..

Kata …………………………...…………… Kijiji ……………………………….…..

Kabila ………………………………………………

Jina la mzazi/mlezi ………………………………………………………………….……………

Kama ni mlezi taja uhusiano………..........................................……………………………………..

Anwani yake ……………………..…………………………………………………………………

Simu ya kazini ……….……………. Nyumbani …………………….. Jirani………...............……..……

Kazi ya mzazi/mlezi …………………...........................................……………………….……..………

Kama ni mfanyakazi taja mahali ………….......................................................………………………..

Anwani ………………………………………………

Endapo kuna dharura aarifiwe ndugu wa karibu aitwaye

…………………………..............……………………..……………………………………………

Ambaye ni (uhusiano) ……………………………………………. Yangu.

Anwani yake ……………………………………………………………………

Simu yake ……………………………………………………………………..

Baba amefariki/hai ……………………….. Mama amefariki/hai……………………

Tatizo la kudumu kama Athma, kisukari, Blood Pressure, Kifafa n.k. ……………………...……………

Je wazazi wapo pamoja au wametengana? ……………………………………………………………

Kama wametengana unatunzwa na nani? ……………………………………………………………

Uhusiano……………………………………………………………………………………………

Taarifa zako za maendeleo zitumwe kwa ………………………………………………………….…

Anwani ……………………………………………. Simu ……………………………………………….

**MKATABA NA KAULI YA KUKUBALI KUTII SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**

Mimi……………………………………………………………………(Jina la mwanafunzi) Ninakiri kuwa nimesoma na kuzielewa vizuri sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoainishwa katika vipengele vyote, na kuwa mara nikiukapo sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe kama zilivyoainishwa dhidi yangu.

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………..

SAHIHI YA MWANAFUNZI…………………………………………..

TAREHE…………………………………………………………………

Mimi ………………………………………………………….(Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi) wa mwanafunzi……………….……………………….(Jina la mwanafunzi) wa kidato cha……………… tahasusi(comb.) ya……………….. Nakiri kupokea, kusoma na kuzielewa taratibu zote zilizo kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Mahida. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakuwa tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi yake na shule. Nitakamilisha mahitaji yote ya shule kwa wakati.

JINA LA MZAZI/MLEZI ……………………………………..…………

Namba za simu…………………………………………………………

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI……………………………………………

TAREHE………………………………………..

Namba ya simu ya ndugu/Jamaa wa karibu…………………………………

| | | | |
|---|---|---|---|
| Picha 1 ya mzazi au ndugu<br>Ibandikwe hapa | Picha 2 ya mzazi au ndugu<br>Ibandikwe hapa | Picha 3 ya mzazi au ndugu<br>Ibandikwe hapa | Picha 4 ya mzazi au ndugu<br>Ibandikwe hapa |

PRIME MINISTER'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## MEDICAL EXAMINATION FORM

❖ To be completed by a medical Officer in a Government hospital.

STUDENT'S FULL NAME: …………………………………………………………………

AGE: ……………………………………………………..

1. Blood count (Red and White): ……………………………………………

2. Stool Examination: ………………………………………………………………

3. Urine Examination: ……………………………………………………………

4. Eye test: ………………………………………………………

5. Ear test: ………………………………………

6. Speech test: ……………………………………………………………

7. T.B  test:  ………………………………………………………………………

8. STD test: ………………………………………………………………………

9. Spleen: …………………………………………………………………………………

10. Abdomen: ……………………………………………………………………………..

11. Additional information from any Physical, Mental, Hereditary diseases or disabilities:

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

*Treatment after Examination:*

…………………………………………………………………………………………………

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above-mentioned student has been thoroughly examined by me and found fit/unfit to pursue further education.

SIGNATURE: ……………………………………………

DESIGNATION/STAMP…………………………………………………

DATE: …………………………………………………………..

STATION: ………………………………………………………